

IDARA YA UTUMISHI WA UHAMIAJI, ZIMAMOTO NA UOKOAJI YAELIMISHA WADAU WAKE KUHUSU MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA NA. 18 YA MWAKA 2007

Imetolewa na Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma

Idara ya Utumishi wa Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji imefanya Mkutano ili kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi na kuangalia mafanikio na mapungufu yaliyojitokeza katika utumishi wa Idara hiyo ili kuweza kuyafanyia maboresho.

Aidha, Idara ya Utumishi wa Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji imetumia fursa hiyo kuwaelimisha wadau wake kuhusu marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na.18 ya mwaka 2007 hususani yale yanayogusa utendaji kazi wa Utumishi wa Idara hiyo.

Mkutano huo umefanyika hivi karibuni katika Mkoa wa Kilimanjaro ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma Bibi. Thecla W. Shangali na kushirikisha wadau wa Idara ya Utumishi wa Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji nchini ambao ni Maafisa Uhamiaji wa Mikoa, Maafisa Uhamiaji Makao Makuu, Makamishna wa Zimamoto na Uokoaji na pia Afisa Mwandamizi kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi.

Wadau wengine walioshiriki katika Mkutano huo ni kutoka Idara ya Utumishi Serikalini na Idara ya Utawala Makao Makuu Tume ya Utumishi wa Umma .

Mkutano huo ulilenga kuelimisha wadau wa Idara ya Utumishi wa Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji kuhusu marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 18 ya mwaka 2007 ambayo yamepelekea Idara hiyo kuondolewa katika usimamizi wa Tume ya Utumishi wa Umma hadi hapo chombo cha kusimamia Utumishi wa Idara hiyo kitakapoundwa.

Washiriki wa mkutano huo wametathmini malengo na kuweka mikakati ya utekelezaji wa marekebisho ya sheria hiyo na namna ya kukabiliana na changamoto zake ili kuboresha utendaji wa kazi wa Idara hiyo hususani katika kipindi hiki cha mpito.

Naibu Katibu wa Idara ya Utumishi wa Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji Bw. Donald S. Ndagula amesema matarajio ya Mkutano huo ni kuwa wadau wataweza kuzingatia sheria, kanuni na taratibu kama ilivyorekebishwa katika Sheria Na. 18 ya mwaka 2007.

Bw. Ndagula ametaja baadhi ya maazimio yaliyopitishwa na wadau katika Mkutano huo kuwa ni Mamlaka za ajira na nidhamu za Idara ya Utumishi wa Uhamiaji na Zimamoto ziwasilishe taarifa za kiutumishi katika Tume ya Utumishi wa Umma moja kwa moja na uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu katika masuala ya ajira na nidhamu.

Pia Idara ya Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji iwe na mpango wa mafunzo unaohusisha watumishi wote na pia ukamilishaji wa sheria na chombo kitakachosimamia Utumishi huo.

Bw. Ndagula amebainisha kuwa Idara ya Utumishi wa Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji ya Tume ya Utumishi wa Umma itaendelea kufanya ukaguzi katika utumishi wa Idara hiyo kufuatia malalamiko mbalimbali yanayojitokeza.

Mkutano huo wa siku mbili umeshirikisha jumla ya washiriki 50 kutoka Kanda ya Kaskazini-mashariki na Kusini ukiwemo Mkoa wa Rukwa, Mbeya, Morogoro, Iringa, Mtwara, Ruvuma, Lindi, Pwani, Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Dar es salaam.

Awali, Idara ya Utumishi wa Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji ilifanya mkutano mwezi Machi mwaka huu katika Mkoa wa Mwanza ili kutathmini utendaji wa kazi wa Idara hiyo na kushirikisha wadau wake kutoka Kanda ya Ziwa na Kati.

Iwapo una maoni/ maswali tafadhali tuandikie

Katibu

Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

S.L.P 9143

DAR ES SALAAM